

Maswali

1. Mariamu na Yusufu walienda wapi kila mwaka?
2. Walienda kusherekea siku kuu gani?
3. Yesu alikuwa na umri gani akienda nao?
4. Yesu alijua nani atakuwa Mfalme Yerusalemu?
5. Nani aliachwa nyuma wakati Mariamu na Yusufu walirudi?
6. Kuna mwenye aliona Yesu kwenye hiyo safari ya kwenda nyumbani?
7. Yusufu na Mariamu walimtafuta Yesu kwa siku ngapi?
8. Walimpata Yesu wapi?
9. Mariamu alimwambia Yesu nini?
10. Yesu alijibu nini?

Majibu

1. Mariamu na Yusufu walienda Yerusalemu kila mwaka.
2. Siku kuu iliyoitwa Pasaka.
3. Yesu alikuwa na miaka kumi na mbili alipoenda nao.
4. Yesu alijua atakuwa mfalme.
5. Mariamu na Yusufu walipokuwa wakirudi, Yesu aliachwa nyuma.
6. Hakukuwa na aliyemuona.
7. Yusufu na Mariamu walimtafuta Yesu kwa siku tatu.
8. Walipata Yesu Hekaluni.
9. Mariamu alisema, “Mbona umefanya hivi.”
10. Yesu alisema, “Lazima niwe kwa shughuli za Baba yangu.”

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

35 Yesu anaenda Yerusalemu

Marejeo

Luka 2:39—52

Kiini cha somo

Kuonyesha vile Yesu alielewa kwamba yeye ni mtoto wa Mungu tangu utoto

Maneno maalum

1. Mariamu + Yusufu + Yerusalemu + Yesu + kumi na mbili + Pasaka + karamu
2. Safari + kaa + nyuma
3. Siku ya tatu + Hekalu + Walimu + Sheria + sitaajabu
4. Kazi ya Baba + Nazareti + Yesu + tii + Mwana kondoo wa Mungu

35.1 Mariamu na Yusufu walienda Yerusalemu kila mwaka kuadhimisha siku kuu ya pasaka. Yesu alipotimiza miaka kumi na mbili aliandamana na Yusufu na Mariamu kwenda Yerusalemu. Yesu alijua huo ulikuwa mji wa Daudi. Alijua wakati utafika atakapokalia kiti cha enzi cha Daudi vile Mungu aliahidi. Kabla ya hiyo lazima awe mwana kondoo wa Mungu wa kuchukuwa dhambi za ulimwengu. Yesu alikuwa akifikiria hii wakati makuhani walikuwa wakiuwa kondoo wa pasaka.

35.2 Karamu ya Pasaka ilipoisha Yusufu na Mariamu waliondoka kwenda Nazareti. Watu wengi walikuwa wameenda Yerusalemu kwa hiyo karamu. Wote waliondoka kurudi.

Yesu alibaki nyuma huko Yerusalemu wakati Mariamu na Yusufu walitoka. Baada ya mwendo wa siku mzima wakakunduwa na kuanza kumtafuta. Waliuliza, “Mmemuona Yesu?”



Hakukuwa na aliyemuona mtoto mvulana Yesu. Ilibidi Yusufu na Mariamu warudi Yerusalemu. Walimtafuta kila mahali lakini walimkosa.

35.3 Hadi siku ya tatu wakiwa na uoga. Wakaenda Hekaluni. Huko kwenye Hekalu walimpata amekaa na walimu wa sheria za Mungu. Alikuwa akiwauliza maswali. Walimu walistaajabu kwa kuona Yesu anajua sana sheria za Mungu.

Mariamu alifurahi sana kumuona na akamkimbilia. “Mwanangu,” alisema, “mbona umetutenda hivi kutuhofisha? Babako na mimi tumekuwa tukikutafuta kila mahali na tumekuwa na hofu.”

35.4 Yesu aligeuka na kumwangukia mama yake. Alijua Yusufu hakuwa Baba yake bali alikuwa Mungu. Aliuliza, “Mbona mnanitafuta? Hamjui inanipasa nifanye kazi ya Baba yangu.” Ndiyo, Yesu alijua kwamba Mungu ndiye Baba yake, na lazima ajue yote yanayomhusu Mungu ndio afundishe watu atakapokuwa mtu mzima.

Yesu aliwatii Yusufu na Mariamu na akarudi nao Nazareti. Alifanya yote aliyoambiwa afanye. Lakini alijua wakati mmoja atarudi Yerusalemu awe mwana kondoo wa Mungu kwa kutolewa kama dhabihu ya dhambi.

